# HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA BAADA YA KULA KIAPO CHA URAIS, TAREHE 18 MACHI, 2021.

***Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,***

***Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Mahakama Kuu ya Tanzania,***

***Mheshimiwa Job Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,***

***Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,***

***Ndugu Bashiru Ali Kakurwa, Katibu Mkuu Kiongozi,***

***Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili;***

***Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne;***

***Viongozi wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama,***

***Ndugu Viongozi wa Dini,***

***Viongozi wa Vyama vya Siasa;***

***Ndugu Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana.***

***Asalaam Aleikum, Bwana Asifiwe, Tumsifu Yesu Kristo.***

***Ndugu Watanzania wenzangu,***

Si siku nzuri sana kwangu ya kuhutubia Taifa maana nimeelemewa na kidonda kikubwa kwenye moyo wangu na mzigo mzito mabegani mwangu. Kiapo nilichokula leo ni

tofauti na viapo vyote nilivyowahi kula katika maisha yangu. Tofauti na viapo vya awali ambavyo nilivila kwa faraja, nderemo, vifijo na bashasha tele. Leo nimekula kiapo cha juu kabisa katika nchi yetu adhimu Tanzania nikiwa na majonzi tele na nchi ikiwa imetandwa na wingu jeusi la simanzi kubwa. Nimekula kiapo katika siku ya maombolezo. Kwa ajili hiyo, mtaniwia radhi kuwa nitaongea kwa uchache na kwa ufupi. Tutatafuta wasaa hapo baadae tusemezane, tukumbushane na tuwekane sawa juu ya mambo mengi yanayohusu Taifa letu, mustakabali wake na matarajio yetu ya siku za usoni. Mniruhusu basi leo niseme maneno machache sana.

Mtakumbuka tarehe 17 Machi 2021 (Juzi) nikiwa Tanga nilipata fursa ya kulihutubia Taifa katika hali ya udharura sana.

Nilitumia fursa ile kuwajulisha juu ya msiba mkubwa ulioifika nchi yetu wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wetu mpendwa na Amiri Jeshi wetu Mkuu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Nikiri kuwa si jambo ambalo nilikuwa nimejiandaa nalo wala kulitazamia. Ni jambo ambalo hatujawahi hata kuwa na uzoefu wala rejea nalo (precedence) katika historia ya nchi yetu. Ni mara ya kwanza tumekuwa na mazingira haya ambayo tumempoteza Rais wa nchi akiwa madarakani. Ni mara ya kwanza pia kwa aliyekuwa Makamu wa Rais kuapa kuwa Rais katika mazingira ya aina hii.

***Ndugu Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Nichukue fursa hii kwa mara nyingine tena kutoa rambirambi zangu za dhati kwa Mama Janeth Magufuli, Mjane wa Hayati Mheshimiwa Rais John Magufuli, Mama Susan Magufuli, watoto na familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na kipenzi chao na mhimili muhimu wa familia. Natambua ukubwa wa ombwe ambalo ameliacha katika familia. Nitumie fursa hii kuwahakikishia kuwa tunaungana nao katika kipindi hiki kigumu cha majonzi na kuahidi kuendelea kuwashika mkono na kuwafariji. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira na ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu. Si jambo jepesi wala rahisi.

Natoa pia salamu zangu za rambirambi kwa wananchi wote wa Tanzania kwa pigo hili kubwa. Ni msiba mzito na ambao hatukuutarajia. Sote tunafahamu namna Hayati Rais Magufuli alivyoipenda nchi hii na alivyojitoa kuwatumikia watu wake. Sote tulishuhudia kiu, dhamira na nia yake njema na ya dhati ya kutaka kuibadili nchi yetu na kuipatia mafanikio makubwa. Sote ni mashahidi wa namna ambavyo ameweza kuibadili taswira ya nchi kwa vitendo na kwa utendaji wake imara, usiotikisika wala kuyumbishwa huku muda wote akimtanguliza Mungu mbele. Sote tulisikia matamanio na maono yake makubwa kwa nchi hii aliyoyatafsiri katika mipango, mikakati na ujenzi wa miradi mikubwa.

Mimi nilipata bahati ya kuwa Makamu wake. Alikuwa ni kiongozi asiechoka kufundisha, kuelekeza kwa vitendo vipi vitu anataka viwe au vifanyike (Elezea kwa ufupi kisa kimoja cha jinsi alikuwa mwalimu kwako). Amenifundisha mengi. Amenilea na kuniandaa vya kutosha. Naweza kusema bila chembe ya shaka kuwa, tumepoteza kiongozi shupavu, madhubuti, mzalendo, mwenye maono, mpenda maendeleo, mwana mwema wa Afrika na mwanamapinduzi wa kweli wa bara hili. Mheshimiwa Magufuli alikuwa chachu ya mabadiliko. Kwa kweli, ***tumepwelea*** kwa kuondokewa na kiongozi wetu huyu***.*** Hatuna cha kusema zaidi ya kusema, '***Raha ya Milele umpe ee bwana na mwanga wa milele umuangazie, ampumzike kwa Amani, amina.”*** Kwa sisi Waislamu tunasema, ***'Inna lillahi wa ina ilayhi raji'un”.***

***Ndugu Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Niwaombe Watanzania tuwe na moyo wa subra, tujenge umoja na mshikamano katika kipindi hiki kigumu. Niwahakikishie kuwa tuko imara kama Taifa na sisi viongozi wenu tumejipanga vizuri kuhakikisha kuwa tunaendelea pale mwenzetu alipoishia. Tunayo Katiba ambayo nimeapa kuilinda na kuisimamia ambayo imebainisha vizuri hatua za kufuata pale inapotokea tukio kama hili la kumpoteza Rais akiwa madarakani. Isitoshe, nchi yetu inayo hazina nzuri ya uongozi na misingi imara ya utaifa, udugu, umoja na ustahamilivu na nidhamu ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama iliyojengwa na viongozi waliotutangulia kwa kuanzia na waasisi wetu Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume. Pamoja nao, Marais

Wastaafu waliofuatia na Mpendwa wetu Hayati Rais Magufuli. Niwahakikishie kuwa ***Hakuna jambo litakaloharibika!***

***Ndugu Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Kabla sijamaliza, nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi wa mihimili yetu muhimu ya Bunge na Mahakama kwa mshikamano waliouonyesha katika kipindi hiki. Nimshukuru Mhe. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na mihimili yake yote kwa kuwa nami bega kwa bega katika kipindi kigumu. Aidha, nawashukuru pia wenzangu katika Serikali wakiongozwa na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa ushiriki wao katika kusimamia kipindi hiki cha mpito. Niwashukuru pia Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama

kwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo chini ya Katiba yetu kwa kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa ya amani na tulivu. Niwashukuru viongozi wa dini kwa kuendelea kuliombea Taifa letu katika kipindi hiki kigumu.

Kipekee, nikishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa ukomavu wake na uongozi wake madhubuti ambao ndio msingi wa kuwezesha mabadiliko haya ya uongozi kwa amani na utulivu. Nitumie fursa hii pia kuwashukuru ndugu zetu wa Vyama vya Upinzani kwa salamu zao za kunitia nguvu, faraja na mshikamano walizonifikishia mara tu baada ya kutangaza taarifa za msiba huu mkubwa. Katika muktadha huo huo, niwashukuru viongozi wenzangu kutoka nchi jirani na nchi rafiki duniani kote waliotufikishia salamu za rambirambi

kutokana na msiba huu mzito. Vilevile, nivishukuru vyombo vyetu vyote vya habari ambao wamekuwa wakirusha matukio yote mubashara bila kuwasahau wasanii wetu ambao wametunga tungo; na nyimbo mbalimbali za faraja. Na mwisho, japo si mwisho kwa umuhimu, niishukuru familia yangu, hususan mume wangu kipenzi, watoto wangu wapendwa, ndugu, jamaa marafiki pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kunitia nguvu na kunifariji katika nyakati hizi ngumu.

***Ndugu Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Kabla sijahitimisha, naomba niwaase ndugu zangu Watanzania kusimama pamoja na kushikamana katika kipindi hiki cha maombolezo. Huu ni wakati wa kuzika tofauti zetu na

kuwa wa moja kama Taifa. Ni wakati wa kufarijiana, kuoneshana upendo, udugu wetu, kudumisha amani yetu, kuenzi utu wetu, uzalendo wetu na Utanzania wetu. Huu si wakati wa kutazama mbele kwa mashaka, bali kwa matumaini na kujiamini. Si wakati wa kutizama yaliyopita, bali wakati wa kutizama yajayo. Si wakati wa kunyosheana vidole, bali wakati wa kushikana mikono na kusonga mbele. Ni wakati wa kufutana machozi na kufarijiana ili tuweke nguvu zetu pamoja kujenga Tanzania mpya ambayo mpendwa wetu Rais Magufuli aliitamani.

Kama nilivyotangulia kusema awali, leo si siku ya kusema sana. Ni wakati wa kuomboleza na kutafakari yale yote mema aliyotufanyia Mpendwa wetu, kipenzi chetu na aliyekuwa Rais

wetu, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Zaidi, tuungane sote kumuombea kwa Mwenyezi Mungu apumzishe roho yake mahala pema, peponi. Amina!

***Asanteni sana kwa kunisikiliza!***